



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**



MKOA WA KILIMANJARO

Simu : 27-29 74369
Fax : 27- 29 74368
Email: ded@haidc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
HAI KILIMANJARO

Kumb.Na.LG/B.20/2/146

Tarehe: 24/01/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai anatangaza **nafasi za kazi ya Mkataba** kwa wananchi wa Tanzania wenye sifa na ujuzi wa nafasi zifuatazo:-

1 MKUSANYAJI WA MAPATO (NAFASI 10)

Sifa za mwombaji:

- Awe na Cheti cha Astashahada ya Uhasibu / Biashara kutoka Chuo kinachotambulika na serikali
- Asiwe mwajiriwa wa Serikali
- Awe na uwezo wa kutumia simu janja (Smart Phone)
- Mwombaji lazima awe mkazi wa Wilaya ya Hai.

Majukumu ya kazi ya Ukusanyaji wa Mapato

- i. Kukusanya mapato/kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali vya Halmashauri kwa kutumia mashine (POS)
- ii. Kuwasilisha taarifa ya makusanyo ya kila siku
- iii. Kuhakikisha mapato/kodi yote yaliyokusanywa yanapelekwa benki na kuingiza kwenye akaunti ya Halmashauri
- iv. Kutunza na kuhakikisha usalama wa mashine ya kukusanyia mapato (POS), risiti za kuweka fedha benki na vitabu vya kuhifadhia kumbukumbu za mapato
- v. Kuhakikisha taarifa ya mapato inaandaliwa katika vitabu maalumu vya taarifa za mapato
- vi. Kutoa risiti halali za EFD kwa walipa mapato/kodi
- vii. Kufanya ulinganishi wa kila siku wa fedha zilizokusanywa na zilizowekwa benki
- viii. Kushiriki katika ulinganishi wa fedha zilizokusanywa na zinazoonekana kwenye POS na taarifa za kwenye mifumo ya fedha ya Halmashauri

- ix. Kubaini na kutoa taarifa ya wakwepaji wote wa kulipa kodi na mapato.
- x. Kuhakikisha mashine ya kukusanyia (POS) inawasilishwa mara kwa mara Halmashauri kwa ajili ya ukaguzi
- xi. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na kazi husika

Mshahara: Ni makubaliano kati ya mwajiri na mwajiriwa

2. MTEKNOLOJIA MSAIDIZI DAWA (Nafasi 2)

Sifa za mwombaji:

- i. Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne wenye Astashahada au Stashahada ya Mteknolojia Msaidizi wa dawa kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali na awe amesajiliwa.
- ii. Awe na elimu ya kidato cha nne
- iii. Awe na uwezo wa kutumia kompyuta

Majukumu ya Kazi

- i. Kuandaa mahitaji na matumizi ya dawa na vifaa
- ii. Kuagiza kuhifadhi na kugawa dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi
- iii. Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba
- iv. Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba
- v. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

Mshahara; Ni makubaliano kati ya mwajiri na mwajiriwa

MASHARTI YA JUMLA:

1. Mwombaji lazima awe Raia wa Tanzania.
2. Awe na Umri wa miaka 18 hadi 45.
3. Awe mwadilifu na asiwe na historia ya uhalifu
4. Waombaji waambatishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimumafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyodhibitishwa na wakili au mahakama
5. Testimonials, provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita (form iv na form vi result slip) havitakubalika.
6. Waombaji waliosoma nje ya nchi waambatishe uthibitisho kutoka mamlaka husika (TCU) wahakikishe vyeti vyao vimekaguliwa nakuthibitishwa na mamlaka husika.
7. Waombaji waambatishe maelezo binafsi.

8. Maombi yote yaambatishwe kitambulisho cha NIDA/namba ya NIDA.

NB: Waombaji wa nafasi ya Mkusanya mapato anatakiwa awe na wadhamini watatu (03) wanaomiliki mali zisizohamishika.


Mwombaji mwenye sifa anatakiwa kutuma maombi kwa anuani ifuatayo:-

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Hai,
3BR-TTCL-Kanisani,
25382. Bomang'ombe,
S.L.P. 27,
HAI KILIMANJARO

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **31/01/2023 saa tisa na nusu alasiri.**

NB:Tangazo hili linapatikana katika tovuti ya Halmashauri www.haidc.go.tz, tovuti ya secretarieti ya ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za matangazo za Halmashauri.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:-


Dionis M. Myinga
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
HAI
MKURUGENZI MTENDAJI (W.)
HAI